UTATHMINI WA UMILISI

GREDI YA 6

MUHULA WA KWANZA 2024

KISWAHILI

JINA: _____TAREHE_____

SHULE: _____

1. **<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.</u>**

Siku tuliyokuwa tumeisubiri kwa hamu na ghamu ilifika. Ilikuwa nisiku ya Alhamisi. Siku yenyewe ilikuwa ya pekee kwani fainali ya mpira wa kabumbu kati ya shule yetu na shule ya Heshima, ingechezwa.Wachezaji wa shule yetu wa pamoja na mashabiki wao walionekana kuwa na furaha tele. Ama kweli, leo ni leo msema kesho ni mwongo.

Wanasoka wa timu ya Heshima walifika mapema ajabu. Huenda walijua kwamba chelewa chelewa utapata mwana si wako. Walionekana wakivinyosha viungo vyao kwa bashasha. Mashabiki wachache waliokuja nao walikuwa na maneno mengi kuliko chiriku.

Kabla ya mechi kuanza, kocha wetu alituita. Alituhimiza kuwa ili kupata ushindi, tulihitajika sote tufanye bidii kama mchwa.

Vile vile, tulistahili kushirikiana kama kinu na mchi na kuziweka nia zetu sote pamoja.

Mechi ilianza taratibu taratibu taratibu tu. Ilikuwa kama kwamba timu zote mbili ziliogopana.

Hakuna mchezaji aliyetaka kulifaya kosa lolote. Kila mmoja alitambua kosa moja tu hasa karibu na goli lao lingesababisha au lingeashiria hatari kubwa sana.

Jinsi muda ulivyosonga ndivyo kasi ya mechi ilivyozidi. Mashabiki wa timu zote nao hawakutulia. Kelele zilizoenea uwanjani hazikuwa na kipimo wala kikomo. Ungedhani kwa mchawi kumeingia mwendawazimu hasa. Ghafla tu, mchezaji wa timu yetu (mahiri) aliupata mpira katika eneno la hatari. Naye hakupoteza muda wowote. Aliudhihirisha umahiri wake kwa kumpiga chenga moja safi sana beki wa Heshima; akamwacha hoi chini. Akamtishia kipa upande wa kushoto na kumbwaga kulia. Goooooooli!'. Akautikisa wavu kwa bao maridadi kabisa.

Uwanja ulipata kelele mara mbili zaidi. Wachezaji wa Heshima wakazidiwa nguvu. Hata hivyo, walijikaza kiume ili kuhakikisha kwamba hawajafungwa bao jingine. Mechi ikakamilika kwa ushindi wa shule yetu; bao moja kwa nunge. Ama kweli, mcheza kwao hutuzwa. Naye asiyekubali kushindwa.....

Kwa nini shule iliyosubiriwa ilikuwa ya pekee?

A. ilikuwa ya Alhamisi
B. ilikuwa fainali ya kabumbu kati ya shule yetu na Heshima.
C. kwa sababu shule jirani ingekuja kwetu
D. kwa sababu ilikuwa ya kucheza

2. Wanasoka wa timu ya Heshima .....

A. Walifika mapema sana
B. Walicheza vyema hadi mwisho wakashinda
C. Walichelewa kufika
D. Walikuwa wa ajabu

3. Timu ya Heshima ilikuja na mashabiki kiasi gani?

A. Wengi waliojaa uwanjani
B. Wenye kelele kama chiriku
C. Wachache wenye maneno mengi